

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**  
DAR ES SALAAM  
Namba ya Simu: 0738166703  
Fax: 255 - 022 – 246011  
Barua pepe:  
[secretary@psc.go.tz](mailto:secretary@psc.go.tz)  
Tovuti: [www.psc.go.tz](http://www.psc.go.tz)



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,  
6 MTAA WA ALBERT LUTHULI,  
KITALU NAMBA 10,  
S.L.P. 9143,  
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU KUANZA KWA MKUTANO  
WA TUME TAREHE 15 HADI 26 MACHI, 2021**

---

Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kufanya Mkutano wa Tatu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 26 Machi 2021. Katika Mkutano huu Tume itapokea na kutolea uamuzi rufaa **99** na malalamiko **06** yaliyowasilishwa na Watumishi mbalimbali wa Umma, ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu katika Utumishi wa Umma.

Shughuli nyingine iliyopangwa kufanyika wakati wa Mkutano huu ni pamoja na kupokea na kujadili, Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma katika kipindi cha Robo ya Pili (Oktoba hadi Desemba, 2020) ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Tume ya Utumishi wa Umma inatekeleza majukumu haya kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma (Sura ya 298 Marejeo ya mwaka 2019).

Imetolewa na:

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Richard M. Cheyo'.

Richard M. Cheyo  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Tume ya Utumishi wa Umma.  
**DAR ES SALAAM**  
12 Machi, 2021